

JINA NAMBARI

SHULE... ..TAREHE

SAHIHI

102/3

KISWAHILI

KARATASI 3 (FASIHI)

KIDATO CHA NNE

JULAI 2017

MUDA: SAA $2\frac{1}{2}$

HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI

MURANG'A COUNTY MOCK

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI

MAAGIZO

- Jibu maswai manne tu
- Swali la kwanza ni la lazima.
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

SEHEMU A:KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA

- Lazima
Kwa kutoa mifano, fafania maudhui ya utu kama yanavyojitokeza katika riwaya ya kidagaa kimemwozea.
(al. 20)

SEHEMU B:MSTAHIKI MEYA – T AREGE

Jibu swali la 2 au 3

- “Mwaka wa kuomba kura utakapofika sitataka mizuka yao kuniandama.”
 - Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
 - Eleza maudhui yanavyojitokeza katika dondoo hili (al.2)
 - Ufisadi uliokithiri ndio uliokuwa msingi wa matatizo ya cheneo. Thibitisha kwa mifano mwafaka(al. 14)
- “Majuto ni mujukuu huja baadaye.” Thibitisha ukweli wa methali hii ukitoa mifano kutoka kwenye tamthilia ya mstahiki Meya. (al. 20)

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O. Box 85726 – 00200, Nairobi

Tel:+254202319748 | +254 733 836593 | email: infosnkenya@gmail.com

Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com

SEHEMU C: USHAIRI

SHAIRI

Hayawihujayakawa, walinena wanenaji
Nyuma walotakwa kuwa, wakawa ndo wajuaji
Nao mbele walokuwa, wakazikosa soseji
Hufika ya wanenaji, hayawi huja yakawa.

Mwendo usimwone waw, damu yake sileleji
Kwa watu akikosewa, kwamba hajipi ujaji
Kimya kikuu angawa, kishindo ukitaraji
Hufika ya wanenaji, hayawi huja yakawa.

Hawanacho walokuwa, huja kuwa wasemaji
Wakawa wanatakiwa, kule wasikotaraji
Hata walioonewa, kama taka za gereji
Hufika ya wanenaji, hayawi huja yakawa.

Hayawi huja yakawa, ulijuwe mjuwaji
Matope waloumbiwa, huziishi za saruji
Na saraji walokuwa, tope likang'ang'aniwa
Hufika ya wanenaji, hayawi huja yakawa.

Mwovu huyo angakuwa, kampe japo kilaji
Sijipe kumumbuwa, hwenda atawale mji
Kiwa hukumtambuwa, jataka ulimjaji
Hufika ya wanenaji, hayawi huja yakawa

4. (a) Andika kichwa mwafaka cha shairi hili (al. 2)
- (b) Taja mbinu mbili za lugha alizotumia mtunzi wa shairi hili (al.4)
- (c) Eleza dhamira ya mshairi (al.2)
- (d) Eleza umbo la shairi hili (al.4)
- (e) Taja methali inayotawala katika shairi (al. 2)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika kwenye shairi
i) ujaji
ii) walotakwa
- (g) Onyesha matumizi mawili ya uhuru wa mshairi (al.2)

SEHEMU D: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

5. Uozo katika jamii ni maudhui yaliyoshughulikiwa pakubwa katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine. Kwa kurejelea hadithi zozote tano fafania kauli hii (al. 20)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI (AL. 20)

6. (a) Eleza istilahi zifuatazo: (al. 12)
 - i) Ayani
 - ii) Misimu
 - iii) Nyiso
 - iv) Mbolezi
 - v) Mbazi
 - vi) Lakabu
- b) Fafania mbinu nne za kukusanya fasihi simulizi (al. 8)

